TANGAZO LA SERIKALI Na. 663 la tarehe. 25/11/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA MPANGO WA URASIMISHAJI WA ENEO LA KITISI YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Mpango wa Urasimishaji wa Eneo la Kitisi ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya urasimishaji.

Mpango wa kina wa eneo

3. Mpango wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi wa Mji wa Makambako.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye njia panda ya barabara ya Njombe – Songea na bomba la mafuta la Tanzania - Zambia - Mafuta (TAZAMA) kwenye alama yenye majira – nukta 700553E, 9021369N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kufuata barabara ya Njombe – Songea kwa umbali wa kilomita 1.633 hadi eneo ambalo barabara za Njombe – Songea na Dar es Salaam – Mbeya zinapokutana kwenye alama yenye majira – nukta 700394E, 9019778N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kwa kufuata barabara ya Dar es Salaam – Mbeya hadi jengo la Ofisi ya Mtaa wa Kahawa kwa umbali wa kilomita 0.614 hadi kwenye alama yenye majira – nukta 699836E, 9020035N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi kwa kufuata barabara ya Kabelege hadi barabara ya mchepuko ya Soko la Kimataifa kwa umbali wa kilomita 0.324 hadi kwenye alama yenye majira - nukta 699594E, 9019818N; baada ya hapo mpaka unaelekea Magharibi kupitia barabara ya mchepuko ya Soko la Kimataifa kwa kufuata barabara ya mtaa kwa umbali wa kilomita 0.667 hadi kwenye alama yenye majira - nukta 699190E, 9020341N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kupitia barabara ya mchepuko ya Soko la Kimataifa kwa umbali wa kilomita 1.583 hadi bomba la mafuta la TAZAMA kwenye alama yenye majira – nukta 699399E, 9021911N; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa kufuata bomba la mafuta la TAZAMA kwa umbali wa kilomita 1.227 hadi ulipoanzia".

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*